

Maswali

1. Mariamu na Yusufu waliishi wapi?
2. Nani aliwambia juu ya ahadi kutoka kwa Mungu?
3. Baba wa Mtoto wa kweli alikuwa nani?
4. Mtoto alikuwa aitwe nani?
5. Mbona Mariamu na Yusufu walitakiwa watoke Nazareti?
6. Yesu alizaliwa wapi?
7. Nani alikuwa wa kwanza kujua kuzaliwa kwa Yesu?
8. Mamajusi waliona ishara gani angani?
9. Walifanya nini walipoiona ?
10. Walimpata aje Mtoto Yesu?
11. Walileta zawadi gani?

Majibu

1. Mariamu na Yusufu waliishi Nazareti.
2. Malaika aliwambia juu ya ahadi kutoka kwa Mungu.
3. Baba wa kweli alikuwa Mungu
4. Mtoto alikuwa aitwe Yesu.
5. Mariamu na Yusufu walitoka Nazareti kwenda kulipa kodi na kuhesabiwa.
6. Yesu alizaliwa Bethlehemu kwenye zizi la ng'ombe.
7. Wachungaji ndio walikuwa wa kwanza kujua kuzaliwa kwa Yesu.
8. Mamajusi waliona nyota angani kama ishara .
9. Walifuata nyota mpaka Israeli .
10. Waliifuata mpaka ilpotua juu ya zizi la ng'ombe Bethelehemu .
11. Zawadi zilikuwa dhahabu, uvumba na manemane.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

34 Kuzaliwa kwa Yesu

Marejeo

Mathayo 1:18—25 na 2

Luka 1:26—56 na 2:1—40

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Yesu alizaliwa

Maneno maalum

1. Nazereti + Israeli + Mariamu + Mama + Yusufu + mme + ahadi + Mungu + Baba + jina + Yesu + Mwokozi
2. Safari + punda + Bethlehemu + kodi na Hesabu + watu wengi + Nyumba ya Wageni + zizi la ng'ombe + nguo
3. Wachungaji + kondoo + kondeni + usiku + nuru kuu + Malaika wengi + imba + zawadi + ona mtoto + abudu + rudi
4. Mamajusi wa mashariki + ishara + nyota + safari + Herode + Yerusalem + Mfalme + mtoto + ibada + zawadi + rudi nyumbani

34.1 Katika nchi ya Israeli kwa mji wa Nazareti, aliiishi mwanamke kijana jina lake Mariamu. Hakukuwa ameolewa lakini alikuwa amepozwa kwa Yusufu.

Kabla waoane Mungu alituma Malaika amwambie ya kwamba alichaguliwa kwa sababu ya kipekee. Mungu alimwahidi kwamba atakuwa na mtoto hivi karibuni. Babake hakukuwa Yusufu lakini Mungu mwenyewe. Hii ingefanyika tu,kwa sababu Mungu angemtumia nguvu isiyo ya kawaida iitwayo Roho Mtakatifu. Mariamu na Yusufu wangemuita huyo mtoto Yesu maana yake 'Mwokozi.' Huyo mtoto hakuwa wa kawaida kwa sababu ye ye ni mwana wa Mungu. Tena angekuwa Mfalme wa ulimwengu wote.

34.2 Mda mfupi ndio mtoto azaliwe, mtawala wa Kirumi aliyekuwa Israeli aliamrisha watu wote warudi walikozaliwa walipe kodi na kuhesabiwa .Mariamu na Yusufu waliitajika warudi Bethelehem kutoka Nazareti na walisafiri kwa siku nyingi.likuwa mwendo mrefu lakini watu wote walifika wakati mmoja.

Mariamu alikuwa amechoka baada ya safari ndefu. Yusufu alijaribu kupata pahali wakae lakini hakukuwa. Walipata pahali wanyama walikaa, katika nyumba ya wageni. Hapa palikuwa na joto, pakavu na paliitwa hori la ng'ombe. Wakati wa usiku Mariamu alizaa mtoto akamvika nguo alizobeba. Alimlaza horini.

34.3 Karibu na hapo kulikuwa na wachungaji wakichunga kondoo zao kondeni. Punde tu, dhidi ya giza kukatokea nuru kuu. Wachungaji wakaogopa sana lakini Malaika aliwatuliza na kuwapa habari njema kuhusu mtoto mvulana aliyezaliwa. waliamuwa waende wajionee kama ni kweli yametokea hivyo. Walipofika Bethlehemu walitafuta hicho chumba cha wageni kulipozaliwa Yesu. Walipompata Mariamu na Yusufu pamoja na mtoto waliinama wakamsudia Yesu na kumpa zawadi. Baadaye walirudi kwenye kondoo wao.



34.4 Kwa nchi ya mbali huko mashariki kulikuwa na Mamajusi waliokuwa wameona nyota angani. Walichunguza chunguza ili wafahamu maana yake kwenye kitabu. Walipopata walisafiri mwendo mrefu wakiifuata nyota mpaka wakafika Israeli.

Kutoka kwa mafundisho walioyasoma, mamajusi walijua kwamba Mfalme alikuwa amezaliwa. Walielekea Yerusalem kwa nyumba ya Mfalme Herode lakini hawakumpata Mtoto. Walieendelea wakiongozwa na ile nyota mpaka kwenye mtoto.

Mamajusi walipoona mtoto Yesu pamoja na Mariamu na Yusufu, waliinama na kumsujidia vile wachungaji walifanya. Walimpa zawadi ya dhahabu, uvumba na manemane kabla ya kurudi nyumbani .

Mariamu na Yusufu walimchukwa Yesu na kurudi nyumbani Nazareti. Walikumbuka juu ya mambo mengi yaliokuwa Bethlehemu.

